Cour
Pénale
Internationale

International
Criminal
Court

Asili : **Kifaransa** N° : **ICC-01/04-02/06**
Tarehe **22/8/2006**

**CHUMBA CHA UTANGULIZI I**

**Kinaundwa na :** **Bwana jije Claude Jorda, jije prezida**
**Bibi jije Akua Kuenyehia**
**Bibi jije Sylvia Steiner**

**Grefye :** **Bwana Bruno Cathala**

**HALI YA MU JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO**
**AFERE**
***PROKIRERE c. BOSCO NTAGANDA***

**Ya siri**

**MANDA YA KUKAMATA**

**Biro ya Prokirere :**
Bwana Luis Moreno-Ocampo, Prokirere
Bibi Fatou Bensouda, makamu wa Prokirere
Bwana Ekkehard Withopf, sibstiti wa kwanza wa Prokirere



PURL: https://www.legal-tools.org/doc/e5736b/

**CHUMBA CHA UTANGULIZI I** ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai («Mahakama»),

**KIKIONA** ombi ya kutoa manda ya kukamata Bosco Ntaganda yenye Mwenye kushtaki alileta siku 13 mwezi ya kwanza mwaka 2006 na tena, ushahidi na mahabari zingine zenye alileta,

**KIKIONA** artikle 19-1 na 58-1 za Mkataba wa Roma,

**KWAKUWA,** kufuatana na ushahidi na mahabari zenye Mwenye kushtaki alileta, afere yenye inaangalia Bosco Ntaganda iko mu uwezo ya kisheria ya Mahakama,

**KWAKUWA** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama vita ya kudumu ilikuwa mu Ituri tangu mwezi ya saba mwaka 2002 mpaka mwisho ya mwaka 2003 na kuendelea,

**KWAKUWA** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama tangu mwezi ya saba mwaka 2002 mpaka mwezi ya kumi na mbili mwaka 2003, batu ya "*Forces patriotiques pour la libération du Congo*" (FPLC) balifanya mara mingi matendo ya kuitika mu jeshi ya FPLC batoto ba miaka chini ya 15 na kubapatia mafunzo mu kambi za mazoezi za FPLC za pale Bule, Centrale, Mandro, Rwampara, Irumu, Bogoro na Sota,

**KWAKUWA** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama tangu mwezi ya saba mwaka 2002 mpaka mwezi ya kumi na mbili mwaka 2003, batu ya FPLC balifanya mara mingi matendo ya kutia mu jeshi ya FPLC ku kinguvu batoto ba miaka chini ya 15 na kubapatia mafunzo mu kambi za mazoezi za FPLC za pale Bule, Centrale, Mandro, Rwampara, Irumu, Bogoro na Sota,

**KWAKUWA** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama mu hii kipindi ya muda yenye imetajwa, batu ya FPLC baliingiza kabisa na tena mara mingi batoto ba miaka chini ya 15 mu mapigano yenye ilifanyika pale Libi na Mbau mu mwezi ya kumi mwaka 2002, pale Largu mwanzo wa mwaka 2003, pale Lipri na Bogoro mu mwezi ya pili na ya tatu mwaka 2003, pale Bunia mu mwezi ya tano mwaka 2003 na pale Djugu na Mongwalu mu mwezi ya sita mwaka 2003,

**KWAKUWA** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama siasa/tabia yenye inazaniwa kama ni ya *Union des patriotes congolais* (UPC) / ya FPLC, yenye ilikuwa ni ya kuitika mu jeshi ya FPLC wala kutia mu jeshi ya FPLC ku kinguvu batoto ba miaka chini ya 15 na kubaingiza kabisa mu mapigano, ilitumiwa mu hali ya vita pale Ituri na kwa kuambatana na ile hali,

**KWAKUWA** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama tangu mwezi ya saba 2002 mpaka siku 8 mwezi ya kumi na mbili mwaka 2003, Bosco Ntaganda, yeye sawa vile makamu wa kiongozi mkubwa wa majeshi ("*chef d'état-major général adjoint*") mwenye kushurulika na operesheni za kijeshi, alikuwa mkubwa wa tatu mu ngazi za cheo za FPLC na, alikuwa anatii tu Thomas Lubanga Dyilo, mkubwa wa bakomanda ("*commandant en chef*") ba FPLC na Floribert Kisembo, kiongozi mkubwa wa majeshi ("chef d'état-major") ya FPLC. Alikuwa mkubwa wa karibu wa bakomanda ya *secteur* ba FPLC na alikuwa na mamlaka ya kisheria na ya matendo ku bakomanda ba kambi za mazoezi za FPLC na bakomanda ba FPLC benye balikuwa banatumika fasi mbali mbali,

**Kwakuwa** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama i) Bosco Ntaganda alikuwa anatumia cheo yake mu FPLC juu ya kutumikisha kabisa siasa/tabia yenye iliundwa na bakubwa ba UPC/FPLC, yenye ilikuwa ya kuitika na kutia mu jeshi ya FPLC ku kinguvu batoto ba miaka chini ya 15 na kubaingiza kabisa mu mapigano, na ii) kama alikuwa anajua kazi yake mu FPLC juu ya kutumikisha ile siasa,

**Kwakuwa** kuko sababu za kutosha za kusadiki kama Bosco Ntaganda alikuwa anaenda mara mingi mu kambi za mazoezi za FPLC kwenye batoto ba miaka chini ya 15 balikuwa banafundishiwa juu bakuwe basoda ya FPLC, na alikuwa moja kwa moja mu mapigano yenye basoda ya FPLC ba miaka chini ya 15 balikuwa ndani kabisa,

**Kwakuwa,** kutokana na sababu zenye zinaandikwa hapa yulu, kuko sababu za kutosha za kusadiki kama Bosco Ntaganda, kufuatana na artikle 25-3-a ya Mkataba, anabeba muzigo ya hizi maefraksyo za kabambi :

i) jinai ya vitani ya kuitika mu jeshi batoto ba miaka chini ya 15, yenye kupewa malipizi kufuatana na artikle 8-2-b-xxvi wala artikle 8-2-e-vii ya Mkataba ;

ii) jinai ya vitani ya kutia mu jeshi ku kinguvu batoto ba miaka chini ya 15, yenye kupewa malipizi kufuatana na artikle 8-2-b-xxvi ya Mkataba wala artikle 8-2-e-vii ya Mkataba ; na

iii) jinai ya vitani ya kuingiza kabisa batoto ba miaka chini ya 15 mu mapigano, yenye kupewa malipizi kufuatana na artikle 8-2-b-xxvi wala artikle 8-2-e-vii ya Mkataba,

**Kwakuwa** kufuatana na artikle 58-1-b ya Mkataba, kukamatwa kwa Bosco Ntaganda kunafaa kwa sasa juu ya kuhakikisha kama atafika mbele ya Mahakama na kama hatazuia maankete wala kuzitia mu hatari,

**JUU YA ILE,**

**KINATOA**

**Manda ya kukamata BOSCO NTAGANDA** mwenye picha yake inasindikiza hii manda, anazaniwa kuwa raia wa Rwanda na kuwa na miaka karibu makumi tatu na tano, anazaniwa kama mbele ya siku 8 mwezi ya munane mwaka 2003 alikuwa makamu wa kiongozi mkubwa wa majeshi (*chef d'etat-major adjoint*) wa FPLC mwenye kushurulika na operesheni za kijeshi za FPLC, anazaniwa kama balimupatiya cheo ya kiongozi mkubwa wa majeshi ya FPLC siku 8 mwezi ya kumi na mbili mwaka 2003, anazaniwa kuwa hii masiku moya mu bakomanda ya *Mouvement révolutionnaire du Congo* (MRC), kundi ya banamgambo benye kufanya kazi yabo mu *district* ya Ituri na kandokando yake tangu mwanzo ya mwaka 2005, na anajulikana tena ku majina ya Bosco Tanganda, Bosco Ntanganda, Bosco Ntangana, Bosco Ntagenda, Bosco Baganda, Bosco Taganda na "le Terminator".

Imeandikwa mu Kiingereza na Kifaransa, ni maandiko ya Kifaransa njo iko na uaminifu.

/saini/
**Bwana jije Claude Jorda,**
**jije prezida**

/saini/
**Bibi jije Akua Kuenyehia**

/saini/
**Bibi jije Sylvia Steiner**

Imefanyika siku ya pili tarehe 22/08/2006
La Haye (Holande)



PURL: https://www.legal-tools.org/doc/e5736b/